



BODI YA MAPATO ZANZIBAR

SHINDANO LA UBUNIFU WA NEMBO RASMI YA MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR (ZRA)

Kwa mujibu wa kifungu cha 4 (1) cha Sheria ya Uanzishwaji wa Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) nambari 11 ya mwaka 2022 kinaeleza Muhuri na Nembo ya Mamlaka katika umbo na namna kama itakavyoamuliwa na Bodi ya Wakurugenzi. Hivyo:

1. Bodi ya Mapato Zanzibar (ZRB) inapenda kuwaalika Wabunifu na Wananchi wote kwa ujumla kushiriki katika Shindano la kubuni Nembo rasmi ya Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ambayo itaelezea kwa upekee na uwazi kazi za Mamlaka.
2. Nembo inatakiwa iwe rahisi kutambulika na kusomeka iwapo itatumika katika maeneo tofauti kama vile Vyombo vya Usafiri, Mabango, Majengo, Tovuti, Mavazi, Mikoba, "Business Card", matangazo ya Televisheni na mitandao ya kijamii pamoja na machapisho mengine.
3. Nembo iwe na jina na rangi zitakazovutia na kujuilikana kwa jina na namba kwenye Kompyuta kwa matumizi kwenye vifaa mbali mbali.
4. **Vigezo vitakavyotumika katika kumchagua Mshindi**
 - a. **Urahisi wa Kutambulika:** Nembo inapaswa kuwa wazi na inayoweza kutambulika kwa urahisi kwa matumizi mbali mbali kama ilivyoelezwa katika kifungu cha 2.
 - b. **Maelezo ya Maandishi na maana yake:** Ubunifu huu unapaswa kuambatana na maelezo ya maandishi ya maana na vipengele vyake; yaani maana ya kila alama iliyopo kwenye nembo.
 - c. **Uhalisia wa Ubunifu:** Ubunifu utakawasilishwa ni lazima uwe halisi na uwe umebuniwa na aliyetuma ubunifu huo na usiwe wa kunakili ubunifu wowote kutoka ndani au nje ya nchi.
 - d. **Uwasilishaji:** Nembo inapaswa kuwasilishwa katika faili za "format" ya PDF, PNG, na JPEG.
 - e. **Lugha:** Maneno yote au alama yoyote itakayotumika inapaswa kuwasilishwa na tafsiri yake katika lugha ya Kishwahili na Kiingereza.
5. **Angalizo**
 - a. Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) itakuwa na haki ya kuisajili Nembo itakayoshinda kama alama yake ya huduma.
 - b. Uamuzi wa Jaji wa shindano hili ndio utakuwa uamuzi wa mwisho.

6. **Zawadi**

Mshindi wa shindano hilo atazawadiwa zawadi ya fedha taslim baada ya Bodi ya Wakurugenzi ya ZRB kuridhia na kuthibitisha na muhusika kuidhinisha juu ya matumizi ya Nembo.

7. **Mawasiliano**

Kila Mbunifu atapaswa kutuma Nembo yake pamoja na barua ya kuwasilisha Nembo hiyo kwa Kamishna Mkuu wa ZRA ikionesha: Jina kamili, picha ya ukubwa wa passpoti ya muhusika, Nambari ya Simu pamoja na anuani ya makazi.

Nembo hiyo itumwe kupitia barua pepe ya zrb@zanrevenue.org kabla ya saa 11:00 jioni ya tarehe 13/01/2023. Barua zote zitumwe kwa anuani ifuatayo:

**KAMISHNA MKUU,
MAMLAKA YA MAPATO ZANZIBAR,
P.O.BOX 2072,
MAZIZINI,
ZANZIBAR.**

Tangazo hili linapatikana pia katika akaunti za ZRB katika mitandao ya kijamii pamoja na tovuti ya ZRB ambayo ni www.zanrevenue.org.